

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

SHULE YA SEKONDARI NKinga,  
S.L.P 292,  
**IGUNGA.**

8/12/2020.

**SIMU Na. 0752304080**

**Kumb: Na. NKSS/2020/01**

Mzazi / Mlezi wa: .....

S.L.P .....

**IGUNGA.**

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKinga WILAYA YA IGUNGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021.**

### **1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kuijunga kidato cha kwanza katika shule hii Mwaka 2020. Shule ya sekondari NKinga, shule ipo umbali wa **Km 81** kutoka Halmashauri ya wilaya ya Igunga. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kufika Shuleni tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **20/01/2020** ndani ya siku kumi na nne (**14**). Baada ya hapo mzazi/ mlezi atakaeshindwa kumuandikisha mwanae atashitakiwa katika mamlaka husika kwa mujibu wa sheria zilizopo.

### **2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

#### **2.1 Sare za shule**

##### **(a). WASICHANA**

- (i). Sketi mbili (2) za rangi ya jani la mgomba, zenyenye Linda box ya nje (**isiwe yenyenye "V"** na iwe ndefu mpaka chini (ifunike soksi).
- (ii). Shati mbili (2) nyeupe (tetroni) mikono mifupi zenyenye nembo ya Shule na tai yenyenye rangi ya kufanana na sketi.
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba (jozi 2).
- (iv). Soksi ndefu nyeupe.
- (v). Viatu vya michezo (raba nyeupe) jozi moja.
- (vi). Hijabu inaruhusiwa iwe ya heshima na ifanane na sare za shule
- (vii). Sweta rangi ya jani la mgomba.
- (viii). T-shirt rangi ya damu yam zee (maroon) yenyenye nembo ya shule kwa ajili ya michezo na shughuli za nje.
- (ix). Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele
- (x). Ufagio wa nje mmoja - **1 (hard Broom)**

##### **(b). WAVULANA**

- (i). Suruali mbili za rangi ya jani la mgomba zenyenye mifuko miwili pembeni na mmoja wa nyuma na ziwe na marinda mawili tu. (modo haziruhusiwi)
- (ii). Shati mbili nyeupe (tetroni) mikono mifupi zenyenye nembo ya shule na tai yenyenye rangi ya kufanana na suruali.
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino wala urembo (jozi mbili) vyenye kamba.
- (iv). Soksi nyeusi
- (v). Viatu vya michezo/raba nyeupe (jozi moja)
- (vi). Sweta rangi ya jani la mgomba
- (vii). T-shirt rangi ya damu yam zee (maroon) yenyenye nembo ya shule
- (viii). Ufagio wa nje mmoja - **1 (hard Broom)**

#### **2.2 Mahitaji muhimu kwa mwanafunzi**

- (i). Daftari kubwa (**Counter Book 3Q**)- 10
- (ii). Kalamu (bluu au nyeusi) za kutosha
- (iii). Mathematical sets (**Mkebe wa hesabu**)
- (iv). Penseli
- (v). Rula
- (vi). Faili moja - 01 (**Plastic file**) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu na mitihani

### **3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na 10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya **Ofisi ya Rais-TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo pamoja na kanuni na taratibu za shule ziliwekwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo unatakiwa kuwa na:-

#### **3.1 ZINGATIA YAFUATAYO**

- (a). Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c). Kuwa katika kila shughuli na nyingine utakazopewa.
- (d). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shulenii.
- (e). Kutunza usafi wa mwili.
- (f). Kuva sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (g). Kuzingatia ratiba ya shule; na
- (h). Kutunza mali za umma.

#### **3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule**

- (a). Wizi
- (b). Uasherati
- (c). Ubakaji
- (d). Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- (e). Kupigana au kupiga
- (f). Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/shule
- (g). Kudharau bendera ya Taifa
- (h). Kuoa na kuolewa
- (i). Kutoa mimba/kusababisha mimba
- (j). Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (k). Kukataa adhabu kwa makusudi
- (l). Kuwa na simu ya mkononi
- (m). Kuwa mtoro

#### **3.3 SEHEMU ZILIZOKATAZWA**

- (a). Kuingia nyumba za kulala wageni (**Guest House**)
- (b). Kumbi za starehe
- (c). Sehemu za kuuzia pombe
- (d). Nyumba za walimu
- (e). Maabara isipokuwa wakati wa kipindi au kibali maalumu

#### **4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na mwanafunzi**

- (a). Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
- (b). Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c). Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**SHADRACK MANASE NKANA  
MKUU WA SHULE**

# **IGUNGA DISTRICT COUNCIL**

**NKINGA SECONDARY SCHOOL,**

**P.O.BOX 292,**

**IGUNGA**

**Date.....**

**Ref. No:.....**

**The Medical Officer (Government Hospital)**

.....

.....

## **PART A:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**Mr/Mrs/Miss..... (Name in full)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time secondary education .The examination should include the following ineligible in case of a defect. Pregnancy (Category 4) will also render a girl ineligible for a secondary education.

1.(a)Eye sight(b)speech(c)Hearing(d)Limb(e)Venereal Deceases (f)Leprosy (g)Epilepsy.

## **PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(a). Eye sight.....

(b). Hearing.....

(c). Speech.....

(d). Limb .....

(e). Venereal Deceases.....

(f). Leprosy.....

(g). Epilepsy.....

2. Neuroses .....

3. Other serious deceases.....

4. Pregnancy.....

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full -time secondary education.

Designation.....Date.....

*Signature &Official Stamp*

**To be completed by a government Officer)**

**NB:** Incase of any serious health problem(s), the records from the

Government Hospital must be submitted to school while reporting.

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

**ANWANI YA MZAZI / MLEZI**

.....  
.....  
.....

## **HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA N KINGA**

Mimi.....Mzazi/Mlezi wa

Mwanafunzi.....aliyekuwa akisoma shule ya  
msingi.....iliyoko katika Wilaya ya.....kwa kuzingatia masharti  
yafuatayo:-

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida nakufanya shughuli zote za kishule akiwa shulenii.
2. Kwamba mtoto wangu nitamtimizia mahitaji yote kama yalivyo ainishwa katika fomu maalum ya maagizo ya kujiunga na shule ya kutwa ya Mwanzugi kwa ukamilifu.
3. Kwamba kwa muda wote huo wote wa miaka minne sitajaribu kabisa kumsumbuu Afisa Elimu Mkoa/Wizara kutafuta nafasi ya bweni bila sababu muhimu.
4. Kwamba mtoto wangu atafuata sheria na kanuni zote za shule wakati wote wa masomo yake kama zilivyo ainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule.

.....  
**Sahihi ya Mzazi/Mlezi.**

Namba ya mtihani.....Jinsia.....

**SEHEMU B.-MWANAFUNZI**

Mimi ..... wa shule ya msingi

.....ninakubali kujeungu na shule ya sekondari Mw nitafuata  
masharti yote na sheria zote za shule.

***SAINI***.....

***TAREHE***.....